

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 880,
Simu: (028) 2988152,
Nukushi: (028) 2988153
Barua pepe: rbckigoma@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113



TAARIFA KWA UMMA

KIGOMA 29/05/2020

ALIYEKUWA MHASIBU MSAIDIZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU
ATIWA HATIANI

Jana tarehe 28/05/2020 Mahakama ya Wilaya ya Kasulu mbele ya Hakimku Mkazi katika Mahakama hiyo **Mhe. CRESENSIA MUSHI**, imemtia hatiani mshtakiwa **TILUMANYWA GEORGE MUZUMA** - aliyekuwa Mhasibu Msaidizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma.

Mshtakiwa TILUMANYWA GEORGE MUZUMA alifunguliwa shauri la jinai Na. CC. 28/2019 na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU - **BONIFACE KAMWESIGILE** mnamo tarehe 25/02/2019 katika Mahakama ya Wilaya ya Kasulu.

Mshtakiwa huyo alishitakiwa kwa makosa ya Kutumia Nyaraka zenye Maelezo ya Uongo Kumdanganya Mwajiri kinyume na kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 na Wizi akiwa Mtumishi wa Umma kinyume na kifungu cha 270 kikisomwa pamoja na kifungu cha 258(2)(a) vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002, hivyo kumwezesha kujipatia fedha kiasi cha shilingi 11,754,000/=.

Katika hukumu iliyotolewa mahakamani hapo, mahakama imemtia hatiani mshtakiwa katika kosa la kwanza la Kutumia Nyaraka zenye Maelezo ya Uongo Kumdanganya Mwajiri kinyume na kifungu cha 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 na kutoa adhabu ya kulipa faini ya shilingi 500,000/= au kutumikia kifungu cha miaka miwili (2) jela.

Mshitakiwa amelipa faini kiasi cha shilingi 500,000/= na kuachiwa huru. Mahakama haikumkuta na hatia mshitakiwa katika kosa la pili.

Awali ilielezwa mahakamani hapo kwamba mnamo mwaka 2012 wakati wa sensa ya Kitaifa ya watu na makazi, mshitakiwa akiwa ndiye mlipaji mkuu wa halmashauri hiyo alikabidhiwa fedha jumla ya shilingi 434,545,000/= kwa ajili ya shughuli za sensa katika halmashauri za Kasulu mjini, Kasulu vijijini na Buhigwe.

Baada ya matumizi na baada ya usuluhishi wa hesabu ilibainika kwamba kiasi cha shilingi 11,754,000/= kilikuwa kimesalia na hivyo kilitakiwa kurejeshwa katika akaunti ya Halmashauri. Mshitakiwa alikatia stakabadhi kuthibitisha kurejesha fedha hizo katika akaunti ilhali fedha hizo hakuzirejesha. Mpaka uchunguzi wa matumizi ya fedha hizo unafanywa na TAKUKURU mwaka 2016/2017 fedha hizo hazikuonekana kwenye kumbukumbu za halmashauri kuwa zilirejeshwa.

*Ofisi ya TAKUKURU inatoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Kigoma kutojihusisha na vitendo vya rushwa na kwamba wanapokuwa na taarifa za vitendo vya rushwa wazitoe taarifa hizo TAKUKURU kwa kufika ofisi ya TAKUKURU iliyo karibu au kwa kupiga simu ya bure **113**.*

Imetolewa na:

STEPHEN P. MAFIPA
KAMANDA WA TAKUKURU (M) KIGOMA
